# MAKALA YA ISIMU JAMI

*YAMEANDALIWA NA BWANA ATAMBA FELIKS*

**Isimujamii** - Ni taaluma inayochunguza uhusiano uliopo baina ya lugha na jamii.

Hasa hushughulikia jinsi watu wanavyotumia lugha katika jamii.

**Isimu**- ni uchunguzi wa lugha kisayansi.

**Jamii** – ni kundi filani la watu wenye uhusiano fulani.

***Mambo yanayoshughulikiwa katika isimu jamii***

i) Tofauti katika lahaja za lugha kama vile Kiswahili cha lamu(kiamu), cha

Mombasa(kimvita), cha unguja(kiunguja), cha bara.

ii) Tofauti katika matumizi ya lugha baina ya makundi tofauti tofauti katika jamii. Mfano

wazee na watoto,vijana na wabunge.

iii) Matumizi ya lugha kutegemea miktadha tofauti kama vile kazini, nyumbani, sokoni, n.k.

iv) Mtazamo wa watu kuhusu lugha. Je, wanaitukuza au wanaitweza?

v) Jinsi mtu anavyotumia lugha kutegemea uhusiano na wazungumzaji au mada husika.

vi) Lahaja mbalimbali za lugha ya Kiswahili.

Umuhimu wa isimu jamii.

i) Huwafunza watu kaida za lugha ili waweze kuitumia ipasavyo kutegemea mila na

desturi.

ii) Humsaidia mzungumzaji au mwandishi kutumia lugha ya Kiswahili kwa ufasaha na

usahihi.

iii) Humpa anayetumia lugha uwezo wa kutambua, kutofautisha na kutumia mitindo

mbalimbali ya lugha kutegemea mahitaji.

iv) Hufunza maadili ya jamii hasa yanayohusiana na matumizi ya lugha kutegemea uhusiano.

Mf. Mtu na mkwewe, mtoto na mzazi, mwajiri na mwajiriwa.

v) Hufunza mbinu za mawasiliano pamoja na mbinu za kupata maana kamili.

vi) Hudhihirisha utamaduni wa jamii.

vii)Humsaidia msemaji au mwandishi kutambua makosa mbalimbali yanayojitokeza wakati

wa kuzungumza au kuandika.

viii) Hufunza mbinu za kuwaelewa watu tunaotagusana nao kwa kuzingatia mambo k.v

hadhi, utamaduni hivyo utangamano.

**Maana ya mawasiliano.**

Utaratibu ambao huwawezesha viumbe kupashana ujumbe ambao unahusisha mwasilishi na

mpokeaji wa ujumbe.

Njia ambazo kwazo mwanadamu huwasiliana.

i) Mgusano na ukaribianaji

ii) Mavazi

iii) Sauti

iv) Ishara za mwili.

**Lugha**

Ni mfumo wa sauti za nasibu zinazotumiwa na wanadamu katika mawasiliano.

***Sifa za lugha.***

i) Hakuna lugha iliyo bora kushinda zingine. –zote ni sawa.

ii) Kila lugha ina sifa zake.

iii) Lugha hubadilika kutegemea mazingira, aina ya tukio, wakati na matumizi ya lugha hiyo.

iv) Lugha ina uwezo kukua, mfano Kiswahili kimebuni msamiati TEHAMA

(Teknolojia ya habari na mawasiliano.)

v) Lugha pia hufa kwa msamiati wake kupotea n.k

***Sababu za kufa/kufifia kwa lugha.***

(i) Lugha moja kusonewa hadhi na isiyoonewa hadhi hufifia.

(ii) Sababu za kiuchumi – watu huishi mijini na kuacha lugha

ya kwanza.

(iii) Lugha kuwa na idadi ndogo ya wazungumzaji.

(iv) Ndoa za mseto.

(v) Kuhamia kwingine – watu huishi na kuingiliana na kundi jingine.

(vi) Melekeo ya watu – wanapoipendelea lugha moja na kuidharau nyingine.

(vii) Kisiasa – Lugha moja kupendelewa kuliko nyingine na viongozi.

***Umuhimu wa lugha.***

i) Hutumika kwa mawasiliano.

ii) Lugha ni chombo ambacho hutusaidia kujieleza na kutoa mawazo yetu.

iii) Hujenga uhusiano baina ya watu.

iv) Ni kitambulisho cha taifa, mtu binafsi na utamaduni.

v) Lugha ni chemchemi ya uchumi mf. Mtangazaji au mwalimu wa Kiswahili.

vi) Huweza kuunganisha watu kama jamii moja.

**Istilahi za Isimu Jamii**

Lugha ni mfumo wa sauti unaochangia kwa mawasiliano ya kimaeneo.

*Msimbo* - Huwa ni lugha ibuka ya kupanga ill kuficha maana.

*Msimu* - Ni lugha inayozungumzwa na kundi ndogo la watu katika jamii. Hasa huibua

misamiati mipya kila uchao.mf. toa chai, dondosha,

*Diglosia* - hali ya kuwa na lugha mbili tofauti katika taifa, zilizo na majukumu tofauti k.m

nchini Kenya Kiswahili ni lugha ya taifa, Kiingereza ni lugha ya ofisini/rasmi.

*Polyglosia* – hali ya kuwa na lugha nyingi tofauti(zaidi ya tatu) katika taifa, zilizo na majukumu

tofauti.

*Lahaja* ni vilugha ambavyo huzalishwa kutoka katika lugha moja kuu, kwa mfano lahaja za

Kiswahili ni kama; kiamu, kipate, kisiu, kijomvu, kimtangata, kiuguja n.k.

*Lafudhi*(accent)

Ni upekee wa mtu kuzungumza.

- Lafudhi ni matamshi ya mzungumzaji yanayojitokeza kutokana na athari za lugha yake ya

kwanza, lugha zinazomzunguka au maumbile katika ala za sauti.

- Mfano: rara badala ya lala, papa badala ya baba.

***Sababu za kuwa na lafudhi.***

(i) Kwa sababu za athari ya lugha ya mama.

(ii) Kwa sababu za athari ya lugha zingine zinazomzunguka mzungumzaji.

(iii) Kwa sababu ya kasoro fulani iliyoko katika ala za matamshi za mzungumzaji.

**Pijini**.

Ni lugha ambayo huzuka katika shughuli za kibiashara au kidini baina au miongoni mwa

makundi yanayotoka maeneo mbalimbali.

***Sifa za Pijini***

· Haina wazungumzaji asilia.

· Huwa sahili na irabu za kawaida.

· Haijakomaa kimsamiati.

· Hukiuka kanuni za lugha.

· Huwa haina wenyeji au wazungumzaji wazawa.

· Hutumia ishara kwa sababu ya uhaba wa msamiati.

**Krioli**.

Ni pijini iliyoimarika na kuwa na watu wanayoizungumza kama lugha yao ya kwanza

***Sifa za krioli***

(i) Huwa na wenyeji kwa mfano; Krioli ya Haiti, Kridi ya Jamaica

(ii) Huwa na miundo thabiti ya kisarufi.

(iii) Huwa na msamiati shabiti unaoweza kutungiwa kamusi.

(iv) Huwa na matumizi mapana katika Nyanja za siasa, muziki, vyombo vya habari na

kadhalika.

**Lugha mame**

Ni lugha asilia ambayo haijaathirika na ingali katika umbo lake asili

Mfano: kifaransa

**Lugha azali**— ni lugha inayozaa lugha nyinginezo.

**Uwili lugha**

Ni uwezo wa mtu kuzungumza lugha mbili.

***Sababu zinazochangia kuwepo kwa uwingi lugha.***

i) Ndoa za mseto

ii) Ujirani wa makabila / mataifa tofauti

iii) Sera za lugha za wakoloni.

iv) Sera za lugha za nchi.-lugha rasmi na lugha ya taifa huweza kuwa tofauti.

v) Mavamizi / vita huwalazimu wananchi kuhamia kwingine hivyo kuwafanya kujifunza lugha

geni.

vi) Dini

vii) Elimu

viii) Umataifa / udiplomasia

ix) Uchumi na biashara

ix) Mwingiliano wa watu katika jamii.

**Aina za uwililugha**

a) Uwililugha sawia

Hii ni hali ya kuwa na uwezo wa kuzimudu zile lugha mbili

b) Uwililugha kupendelea

Ni hali ya kuwa na mwegemeo wa kuionea fahari mojawapo ya lugha unazozijua

c) Uwililugha kupokea

Hii ni hali ya kujibu lugha moja kutumia nyingine, kwa mfano mtoto anapozungumziwa

kiingereza akajibu kwa Kiswahili

d) Uwililugha uliolala

Ni hali ya kuwa ugenini na kulazimika kuisahau lugha yake kwa muda.

e) Uwililugha mfu

Ni hali ya lugha moja kumezwa au kufifia na kutotumika tena.

**Eleza maana ya Lingua Franka.**

Ni lugha inayotumiwa na watu walio na lugha tofauti kwa ajili ya mawasiliano kwa mfano

Kiswahili katika eneo la Afrika Mashariki.

***Sifa za Lingua Franka.***

- Huwa ni lugha ua mawasiliano kati ya watu wenye lugha zaidi ya moja.

- Yaweza kuwa lugha ya kwanza ya mzungumzaji au lugha ya pili na kwa watu wengine lugha

ua kigeni

- Hukiuka mipaka ya kitamaduni

- Hukutanisha watu wa asili mbalimbali.

- Hukiuka mipaka ua kimaeneo - inaweza kutumiwa katika maeneo mapana.

- Hutumiwa na watu ambao lugha zao za mama ni tofauti.

Umuhimu wa lingua franka

- Huleta ushirikiano katika nyanja mbalimbali kama vile, kibiashara, kiuchumi, kielimu, kidini

nk

- Huleta umoja miongoni mwa watumiaji wake hasa wale wenye tamaduni tofauti

- Hurahisisha mawasiliano hasa katika jamii inayogawika katika misingi ya lugha.

***Njia za uzambazaji wa linguafranka***

(i) Vita- kwa mfano lugha ya kigiriki iliweza kueneza kupitia vita. Kifaransa pia kilienezwa

kupitia vita hasa wakati wa utawala wa Napoleon Bornaparte

(ii) Biashara- kisawhili kimeweza kuenea kutokana na dhima yake katika biashara

(iii) Ukoloni- kifaransa, kiingereza na kireno zimeweza kuenea kupitia utawala kama nyenzo

(iv) Elimu- lugha kama kiingereza zimeweza kuenezwa kwa kutumika kwenye mafunzo katika

nchi nyingi za ulimwengu

(v) Nguvu za kisayansi na teknolojia- Nguvu za kisayansi na teknolojia za Amerika

zimechangia kuenea kwa kiingereza katika ulimwengu hasa kwa sababu ya istilahi mpya

zinazoibika kila uchao.

Msimu- semi za mda zinazotumika na kikundi fulani cha watu na hutoweka kwa baada ya mda.

*Eleza tofauti kati ya kuchanganya ndimi na kuhamisha ndimi.*

i). Kuchanganya ndimi – hali ya kutumia zaidi ya lugha moja katika mawasiliano . matumizi

haya hujikita katika sentensi moja / mzungumzaji anatoka kidogo katika lugha moja na

kuingilia nyingine kasha akarejelea lugha awali.

ii)Kuhamisha ndimi – kubadilisha mkondo wa mazungumzo kutoka lugha moja hadi

nyingine ambapo msemaji ana umilisi wa zaidi ya lugha mbili.

*Andika sababu nne za kuchanganya na kuhamisha ndimi.*

- Kupungukiwa na msamiati wa kutumia

- Kujitambulisha na kundi fulani la watu mf waliosoma, wanahirimu n.k

- Kujihusisha na lugha inayoenewa fahari

- Kutaka kuonyesha kuwa una uwezo wa kutumia lugha mbili au zaidi

- Kutaka kufafanua dhana fulani k.muyoka (x-ray)

***Huku ukitoa mifano mwafaka, fafanua kaida tano katika jamii ambazo matumizi ya lugha***

***hutegemea.***

*.*

(i) Mazingira/muktadha.

Hutegemea mazingira ya wazungumzaji k.v. ofisi, sokoni, mahakamani,

kanisani n.k.

(ii) Umri

Vijana wana namna ya kutumia lugha inayojihusisha na mitindo mipya tofauti na

wazee wanaotumia msamiati wenye hekima na ushauri

(iii) Uhusiano

Kuna mahusiano ya aina nyingi, kwa mfano mtoto atatumia lugha kwa njia tofauti

katika kuwasiliana na wazazi wake tofauti na vile atazungumza na watoto wa rika lake

(iv) Jinsia/ uana

Unyenyekevu hujitokeza katika mazungumzo ya wanawake ambayo ni tofauti nay a

wanaume. Lugha ya wanaume huwa na fujo, kiburi na hali ya kutojali sana.

Wanawake watajikita katika mapambo ilhali wanaumewatajikita katika siasa.

(v) Madhumuni/lengo.

Lengo la mzungumzaji humlazimu kuchagua mtindo atakaoutumia kuufikisha ujumbe

wake.

(vi) Mada

Swala linalozungumziwa hulazimu mtu kuteua msamiati unaohusiana na mada

yenyewe.

Kwa mfano, iwapo ni kuhusu kilimo, msamiati wa ukulima

utatamalaki mazungumzo

(vii) Hali ya mtu

Mgonjwa atazungumza kwa upole wakati mlevi atazungumza kiholela bila kuchagua

maneno

(viii) Cheo cha mtu/ hadhi

Madaraka ya mtu huchangia msamiati wa kutumia. Hali ya kuamuru hujitokeza

katika lugha ya waajiri ilhali upole na adabu hutumiwa na waajiriwa.

(ix) Utabaka

Hadhi ya mzungumzaji inaweza kuathiri uchaguzi wa msamiati.

Watu wa tabaka la juu watapenda kuchagua maneno ya kifahari ilhali wale wa tabaka

la chini watatumia maneno ya kawaida.

**TANBIHI:** Kaida katika matumizi ya lugha husababisha kuwepo kwa sajili tofautitofauti katika

miktadha mbalimbali.

**Sajili za isimujamii**

Katika isimujamii, kuna sajili ainati ambazo zina sifa za kipekee ambazo huwa na umuhimu

wake k.m

a) Sajili ya mahakamani

b) Sajili ya biashara

c) Sajili ya maabadi

d) Sajili ya mtaani/vijana

e) Sajili ya hospitali

f) Sajili ya kitaaluma

g) Sajili ya nyumbani

h) Sajili ya biashara.

i) Sajili ya matangazo ya mpira

j) Sajili ya bungeni.

**i. Sajili ya mahakamani**

Soma kifungu kifutacho:

*Kwa mujibu wa sheria kifungu nambari 3 sehemu ya A ya sheria za nchi, umepatikana na hatia*

*ya kutatiza utulivu wa raia wapenda amani kwa kuwatusi na kutisha kuwapiga. Kiongozi wa*

*mashtaka amethibitisha haya kwa kuwaleta mashahidi ambao wametoa ushahidi usiotetereka*

*kuhusu vitendo vyako katika tukio hilo. Korti hii imeonelea una hatia na imeamuru ufungwe jela*

*kwa muda wa miaka miwili bila faini ili liwe funzo kwako na kwa wenzako wenye tabia kama*

*zako. Una majuma mawili kukata rufani.*

***Sifa za sajili hii***

a. Msamiati teule-Jela,rafani,mashtaka,sheria, kiongozi wa mashtaka, mashahidi,

Hakimu jaji, mhalifu,Washikadau / wahusika - kwa mfano

b. Sentensi ni ndefundefu kimuundo.

c. Kurejelea vifungu vya sheria za nchi.

d. Lugha ya hakimu niya kuamuru.

e. Matumizi ya lugha ya heshima/unyenyekevu mf mheshimiwa kurejelea jaji.

f. Matumizi ya maneno ya kukopa/kigeni mf nole proseque, amicus curie nk.

g. Lugha rasmi hutumika.

h. Lugha dadisi hutumika haswa pale mwendesha mashtaka humhoji mshukiwa.

i. Lugha sanifu imetumika kila neno linalotoka kinywani na muundo wa sentensi

huwa na umuhimu wake katika kesi.

j. Lugha iliyotumika ni ya mfululizo - Hakimu anapotoa hukumu hakatizwi.

**Sajili ya darasani/shuleni/ofisi shuleni.**

(i) Sentensi ndefu – (atoe mifano katika hoja zote.)

(ii) Huwa na mwanzilishi mkuu.

(iii)Msamiati ya taaluma mbalimbali.

(iv)kurejelea mawazo ya wengine.

(v) Lugha ya heshima/adabu.

(vi)Kuna urasmi wa lugha

(vii) Lugha iliyo na mbinu au ataratibu maalum;kwanza,kuongezea na mwisho kabisa....

<u>**Sajili ya biashara.**</u>

Ponda mali: Karibu! Wamama wang'are mali safi ambayo huwezi kupata

popote duniani.

Amina: Unauzaje hilo rinda?

Ponda mali: Bei ni kusikilizana, hatuwezi kukosana.

Amina: Nitakupaa shilling hamsini, naona ni mtumba.

Ponda mali: Mama hilo rinda ni original kutoka Marekani kwa meli.

Amina: Nitaongeza shilingi kumi basi.

Ponda mali: Ongeza kidogo, usiniue.

***Sifa za sajili ya biashara***.

(i) Inaeleza ubora wa bidhaa.

(ii) Kuna kupiga chuku k.mhuwezi kupata popote duniani.

(iii)Ina ushawishi.

(iv)Haizingatii kanuni za sarufi – wamama.

(v) Kuchanganya ndimi – original.

(vi)Hutumia lugha ya mkato.

(vii) Hujaa porojo.

(viii) Hutumia lugha nyepesi.

## Sajili katika muktadha wa usafiri.

Aziz: Ingia 46! Adams mbao Kenyatta, railways beba! 46 Adams mbao Kenyatta,

railways!

Shiku: Namba nane ngapi?

Aziz: Mbao ingia, blue.

Shiku: Nina hashuu

Aziz: Blue Auntie

Shiku: Sina

Aziz: Ingia. 46 Adams mbao, Kenyatta railways gari bebabeba.

Ahendera: Mmi sinako shirini. Chukuako tu kumi.

Aziz: Dinga inakunywanga petrol mzee.

Ahendera: Kumi mingi.

Aziz: Haaya ingia twende. Dere imeshona twende. Beba mbele.

### *Sifa za sajili katika muktadha ya usafiri*

i. Kuna matumizi ya lugha maalum k.v 46, ingia twende.

ii. Kuna kitaja vituo mbalimbali ambako gari litapitia.

iii. Ni lugha ya kuchanganya ndimi k.v driver

iv. Inatumia misimu k.v hashru, dinga n.k

v. Haizingatii sarufi k.minakunywanga, sinako n.k

vi. Hutumia sentensi fupifupi

vii. Ina ucheshi mwingi.

## Sajili katika kituo cha polisi.

Ali: Wee kuja hapa. Wewe ni nani? Sema haraka!

Ebo: Mmi ... ni ... afande ni Ebo

Ali: Unatoka wapi sa ii? Hapa hakuna sheria?

Ebo: Samahani mkubwa. Mmi niku...

Ali: Mkubwa wa nani? Wakubwa wako ofisini.

Ebo: Pole mzee.

Ali: Mzee gani? Hii mtu lazima niiwekwa store. Yaani self-contained.

Toa viatu.

Ebo: Tafadhali Bwana Askari, nilichelewa ...

Ali: Mmi sitaki hadithi! Hizo pelekea nyanya yako, eh. Fanya haraka!

Ebo: Naomba mkubwa ...

Ali: Hapa si kanisani. Unaomba! Hata ...

***Sifa za sajili katika kituo cha polisi***

- Lugha yenye ukali kw. Polisi.
- Lugha ya kudhadisi/maswali ni majibu.
- Kuchanganya ndimi.
- Lugha isiyozingatia kanuni za kisarufi.
- Lugha ya unyenyekevu kwa mshukiwa.
- Lugha ya kuamrisha.
- Lugha inayoeleweka kwa urahisi
- Lugha ya misimu.

**Sajili ya maabadini.**

“Ndugu na madada, sote tumealikwa katika karamu hii ya Bwana kabla ya kujongea mezani

pake, Bwana. Pana haja ya kutakasa nyoyo zetu na kujutia madhambi yetu. Sisi sote ni

watenda dhambi na inastahili kumwendea ili aweze kutuondolea madhambi yetu.”

***Sifa za sajili ya maabadani***

(i) Matumizi ya msamiati maalum kwa mfano:

Mungu asifiwe.

Biblia.

Alhadulillahi!

Shetani ashindwe!

(ii) Matumizi ya sentensi refu ili kuweza kueleweka vizuri na waamini.

(iii) Matumizi ya ukale wa lugha-jinsi ilivyoandikwa.

(iv) Kudondoa kauli yaani kurejelea sehemu fulani katika maandiko matakatifu.

(v) Uradidi wa maneno kurudiarudia maneno kama:

Mungu yu mwema

Mwenyezi Mungu

Amina n.k.

(vi) Matumizi ya ishara na miondoko.

Anapohubiri hutumia ishara na miondoko mfano kuinua mkono,

Kuruka kutoka

hapa na pale.

(vii) Kuchanganya nyakati sana kwa mfano: naye akaondoka hapo waende upande wa

mashariki.

(viii) Matumizi ya maneno yenye asili ya kigeni kwa mfano: majina ya wahusika Sila

na Petero.

(ix) Matumizi ya lugha maalum kama vile tamathali za usemi, taswira, jazanda n.k.

(x) Mwelekeo mkubwa wa kunukuu vifungu kutoka vitabu vitakatifu k.v Biblia na

Koran

**Sajili ya hospitali**

KCSE 2010

*"Benki yenyewe haina kitu ... CD4 count yake iko chini ... Ni emergency ... Tutampoteza*

*ikikosekana."*

(a) Taja sajili inayorejelewa na maneno haya. (alama 2)

Sajili ya hospitali/hospitalini/matibabu/kituo cha ya

/zahanati/udaktari/uuguzi/uganga/uganguzi/utabibu/tiba/daktari/tabibu

(b) Fafanua sifa nne zinazohusishwa na sajili hiyo. (alama 8)

i) Kuna matumizi ya msamiati maalum/maneno teule ya kunywa mara mbili

x3/uyoka/exrei/machela n.k

ii) Matumizi ya vifupisho mf CD4/v.c.t

iii) Matumizi ya lugha mseto/kuchanganya ndimi

iv) Kubadili au kuhamisha ili kufanyiwa msingo.

v) Kuna kudadisi/kuuliza maswali/kuhoji/mahojiano/Dayolojia/kusaili/majibizano

m.f Daktari: ulianza kuugua lini? Mgonjwa:

vi) Kutohoa oparesheni benki

vii) Matumizi ya kauli fupifupi/sentensi fupifupi/lugha ya mtaa mf. jina lako? Umri wako?

viii) Matumizi ya lugha maagizo/Tahadhari/masharti/kuliwaza/ushawishi/ unyenyekevu/

ushauri mf.usitumie pombe

ix) Maneno huwekwa wazi/lugha ya ufafanuzi/maelezo ya ndani zaidi mf. Nilipata

ugonjwa kutoka umalaya.

x) Lugha ya usiri m.f Daktari/madaktari huwa na lugha yao isiyoeleweka na

mgonjwa/lugha fiche/matumizi ya mafumbo.

xi) Kuna lugha ya kitaaluma mf CD4 count

xii) Wahusika hurejei wa kwa majina au vyeo. mf. Bw Daktari

xiii) Matumizi ya lugha ya hisia, mf mgonjwa kutoa usiahi kwa sababu ya maumivu.

xiv) Lugha ya mdokezo ulisema ulianza.

xv) Lugha ya matumizi ya usemi halisi

xvi) Matumizi ya lugha ya kwa moja/ana kwa ana

xvii) Matumizi ya ishara/miche 1 x 1/hisabu picha au alama n.k

**<u>Sajili katika muktadha wa siasa.</u>**

*Wananchi, mimi sina mengi. Hapana katika nyinyi asiyenielewa. Sina la kusema, ila*

*ninawakumbusheni kuwa mnahitaji kiongozi atakayeshughulikia maslahi ya taifa zima. Mtu*

*huyo ni mimi na ninajitahidi niwezavyo kujenga masoko, barabara, shule zaidi na mazahanati*

*na maisha yenu yatakuwa ya raha zaidi.*

***Sifa za sajili ya siasa***.

i. Imejaa propaganda k.v. Fulani ni muaji ( bila idhibati)

ii. Ina ucheshi mwingi k.v. rais na mpira aingize bao

iii. Lugha imejaa mafumbo. Yaani ni fiche k.v. ina vitendawili vinategwa

iv. Istilahi maalumk.v kura, mgombea. Demokrasia, katiba

v. Lugha huzingatia mbinu za tawasifu- majisifu kuhusu matendo bora ya mtu.

vi. Lugha shawishi inayovutia wafuasi wengi k.v tafadhali nawasihi mnipigie kura

vii. Ina chuku k.v ahadi nyingi zisizoweza kutimizwa zote

viii. Mjadala uwepo wakati mwingine.

ix. Huweza kuchanganya ndimi kwa kutumia lugha mbalimbali.

x. Mara nyingi sarufi haizingatiwi.

xi. Huwa na kukatizana kauli kutokana na kupiga makofi, vigelegele au kutokubaliana

kwa kauli Fulani.

xii. Lugha yenye matusi hasa wanaporejelea maadui/wapinzani wao.

xiii. Msamiati wa heshima hutumika haswa wanaporejelea wananchi.

**<u>Sajili ya bungeni</u>**

*...napinga hoja iliyotolewa na waziri wa Finance ya kupiga marufuku matumizi ya plastic*

*bags. Baada ya kumsikiza kwa makini, ningependa kumkosoa kwa kudhihirisha kuwa...*

*kulingana na kifungu nambari ...*

***Sifa za sajili ya bungeni***

i. Kuchanganya msimbo/ndimi katika mijadala, ili kujieleza vyema – waziri wa Finance.

ii. Lugha ya adabu – naingependa kumkosoa.

iii. Msamiati na istilahi huhusiana na bungeni k.m vikao vya bunge, spika, mesi, karani –

hoja, kifungu nambari n.k.

iv. Hurejelea sheria za nchi au katiba katika kutetea hoja fulani inayojadliwa.

v. Lugha ya heshima katika mawasiliano na majadiliano-

Mheshimiwa spika

vi. Wabunge hutaja msamiati unaorejelea sheria na kanuni za bunge wanapojadiliana

kuhusiana na maswala mbali mbali, hasa shughuli za kinidhamu.

vii. Lugha huwa sanifu.

viii. Huwa na urudiaji wa maneno mfano. Bwana Spika.

ix. Huwa na kukatizana usemi mfano pale ambapo mbunge husimama kwa hoja ya nidhamu.

x. Mara nyingi huwa na sentensi ndefu ndefu.

**Sajili ya hotelini.**

*Nani kuku.....? Sosi poa leo ...... Mate ndo! ndo! ndo!. Ukimanga hii hutaona daktari kwa miaka*

*kumi...... Ng'ombe je? nani? ......nani!... Ni wewe....... poa basi naja............*

***Sifa za sajili ya hotelini***

i. Matumizi ya maneno au kauli ambazo katika mazingira mengine haziwezi kuwa na

maana nani kuku?

ii. Ng'ombe je?

iii. Matumizi ya msamiati maalumu wa hotelini kwa mfano,

i) Karanga ii) 'Ng'ombe' iii) Chipo iv) Chapo

iv. Lugha ya ucheshi na utani

v. Matumizi ya misimu ukikimanga / surwa

vi. Kuchanganya ndimi

vii. Lugha isiyo sanifu k.m Ukimanga

viii. Tanakali km mate ndo... ndo... ndo...

ix. Matumizi ya sentensi fupi fupi.

**<u>Sajili ya simu</u>**

*"...ah...naomba kumwongelesha Chucho...Naam, naam Chucho*

*Hujambo?...si ...sina neno...naam Mjomba amezidiwa si wa maji si wa chakula...*

*kweli?...Muuguzi mkuu amedhihirisha...Yes...ok...yeah...Ala! Ameishiwa na pesa.*

***Sifa za sajili ya simu***

i. Hutumai sentensi fupifupi ili kuokoa wakati mf. Naam

ii. Huendeleza majibizano mf. Majibizano kati ya Chucho na anayepiwa simu.

iii. Hutumia mbinu ya takriri mf. Chucho, naam

iv. Huhusisha kuchanganya ndimi mf. Kiingereza yes, yeah

v. Aghalabu kanuni za lugha hukiukwa mf. Kumwongelesha

vi. Hulenga moja kwa moja kiini cha habari k.m Baada ya maamkuzi, anamweleza kuhusu

siha ya mjomba moja kwa moja.

vii. Kukatana kalima

viii. Matumizi ya maamkuzi

**<u>Sajili ya michezo.</u>**

*Anachukua ile ngoma kijana Rooney,*

*Kwake chicharito...anachenga moja , mbili*

*Hatari! Hatari! Hatari kwenye lango…*

***Sifa za sajili ya michezo***

i. Kuna kuchanganya ndimi na kubadilisha ndimi.

ii. Matumizi ya msamiati maalum wa michezo.

iii. Hukiuka kanuni za kisarufi/ kuiboronga sarufi

iv. Hutumia mbinu ya utohozi.

v. Matumizi ya lugha ya mkato

vi. Matumizi ya uradidi wa maneno au kauli fulani

vii. Matumizi ya misimu.

viii. Matumizi ya lugha ya taharuki.

ix. Matumizi ya majisifu mengi

x. Kuna kutajataja majina ya wachezaji.

<u>Sajili ya matangazo/ habari/ripoti/radio.</u>

*Mfanyikazi mmoja wa nyumbani amefikishwa mahakamani katika kaunti ya Maganyakulo*

*kujibu tuhuma za kumbaka kikongwe. Mwendesha mashtaka wa polisi bwana Maliza*

*Twende alisema. Mkaka na Makarne alifumaniwa na mshtakiwa alipelekwa rumande hadi*

*septemba 21 mwaka huu ambapo kesi hiyo itatajwa tena. Licha ya hayo, wengi wanadokeza*

*kuwa Huenda adhabu ya kosa hilo ikuwa ni kifo au kifungu cha maisha. Mshtakiwa aliomba*

*apewe dhamana na Serikali ili aachiliwe huru. Hatimaye ombi hilo halikukubaliwa kwa kuwa*

*mfanyikazi huyo hakuwa na mdhamini. Muhimu ni kuwa baada ya kesi hiyo kuamuliwa,*

*mshtakiwa anaweza kukata rufaa katika mahakama kuu. Naye mlalamishi ameomba Serikali*

*impe ulinzi kutokana na kuvamiwa na washirika wa mshtakiwa...*

***Sifa za sajili hii***

i. Huwa na lugha nyepesi

ii. Sentensi aghalabu huwa ndefu ndefu

iii. Hufuata kanuni za usarufi wa lugha

iv. Huhusisha maelezo ya kina ili kuweka wazi yaliyojiri

v. Mara nyingi hutumia wakati uliopita

vi. Wakati mwingine huhusisha wadhamini.

**Sajili ya magazetini.**

*...ya leo ni kuwapa pole wanaofuata na kuenzi makala ya Burudani,toleo la kila*

*Ijumaa.Mwanamziki huyu aliteka nyoyo za wapenzi wa mtindo huu wa mziki.Kwa kweli ya*

*Muumba hufumbwa tu!Mnapoyasoma wakumbukeni jamaa na wapenzi wa nyimbo zake.*

***Sifa za sajili ya magazetini***

i. Hutumia usemi halisi sana

ii. Huchanganya njeo.

iii. Huchanganya ndimi.

iv. Hutumia vifupisho-Shirika la REUTERS.

v. Lugha hupiga chuku

vi. Wakati mwingine husheheni sifa.

**<u>Sajili ya vijana.</u>**

*Niaje wasee! Ma-holiday ndizo hizo tena. Najua ma-mission ni mingi! Lakini jo !*

*Mambo imebadilika ! Ni kubaya maze. Usifikirie kila kitu unaona ni reality, ukadhani ni*

*gold ! Hiyo siyo real life maze ! Round hii maze ni "Ku-chill!" Usipige ma-stunts*

*zingine zitakuacha uki-regret later! NI POA KU- CHILL au aje maze?*

***Sifa za sajili ya vijana***

i. Kubadilisha msimbo –usifikirie kila kitu unaona ni reality.

ii. Si lugha sanifu-Najua ma-mission ni nyingi lakini jo, mambo imebadilika

iii. Matumizi ya sheng- Ma-mission

a. Ku-chill

b. Uki-regret

iv. Matumizi ya sentensi fupi- Ni kibaya maze

i. Ni poa kuchill

v. Kuchanganya msimo-Kuchill ;Ukiregret ;Ma-mission.

vi. Kuna kukatizana kauli.

*Sababu za vijana kutumia lugha hii.*

i. Ukosefu wa msamiati.

ii. Kukubalika katika kikundi fulani.

iii. Kujitambulisha na lugha fulani au kuonyesha umahiri katika lugha zote mbili.

iv. Kufahamu lugha zaidi ya moja.

v. Sheng` ni lugha legevu(rahisi).

vi. Kuipa lugha ladha(kiswahili sanifu hakina ladha)

vii. Ili kuficha ujumbe.

viii. Kujitambulisha na wanahirimu.

***Sifa za sheng`***

i. Huwa na msamiati maalumu unaotumiwa na vikundi vya watu wenye sifa au tabia fulani.

ii. Hujumuisha maneno mapya na maneno ya kawaida.

iii. Aghalabu haijali sheria za kisarufi.

iv. Msamiati wake huwa finyu na chakavu.

v. Maneno husika hupewa maana mpya zilizo tofauti na zile zilizozoeleka katika lugha

nyingine.

vi. Aghalabu huwa mchanganyingo wa lugha nyingi.

vii. Kuna ufupishaji wa maneno na sentensi

*Sifa zinazoifanya lugha ya sheng` isiwe lugha ya taifa.*

i. Kubadilikabadilika kwa msamiati.

ii. Si lugha sanifu.

iii. Haizungumziwi na watu wengi

iv. Hasa ni vijana

v. Sio lugha ya mama ya kikundi Fulani katika nchi

vi. Basi haitajulikana kwa urahisi.

vii. Muundo haufananai na baadhi ya lugha za kwanza za kabila Fulani.

viii. Si lugha ya kienyenji.

*Athari za Sheng'*

1. Huweza kuathiri namna mwanafunzi anavyojieleza katika mahojiano ya kazi.

2. Kukuza matumizi ya lugha legevu katika maongezi na maandishi.

3. Kupotosha ujumbe km. pesa pap!

4. Kielelezo kibaya kwa jamii nan chi kwa ujumla km. kuonyesha nchi isiyo na sera bora ya

lugha.

5. Ni njia ya kufifisha uzalendo wa kujivunia lugha ya taifa.

6. Ni msimbo wa kuficha maovu. Inaweza kutumiwa na vijana kutekeleza maovu. kmuna

mozo/unga (sigara)

7. Huchangia katika alama duni kwa mtihani.

**<u>Sajili ya mazishi /matanga /kilio masikitiko /msiba/ maombolezo/uzikaji.</u>**

*...sote tunajua kwamba ni kudura. makiwa!*

***Sifa za sajili ya mazishi***

i. Msamiati maalum kwa mfano makiwa marehemu.

ii. Lugha ya kufariji/liwaza

iii. Yenye matumaini

iv. Matumizi ya vihihisishi oh, wuui,

v. Lugha ya kusitasita

vi. Huhusisha sana mambo ya kidini na Mungu na Imani za jamii.

vii. Ni lugha ya hasira.

viii. Kuchanganya ndimi

ix. Inaadaman na viziada lugha

x. Matumizi ya sentensi fupi

xi. Matummizi ya sentensi ndefu

xii. Imesheheni sifa za mwendazake

xiii. Matumizi ya lugha isiyozingatia kanuni za kisarufi.

**<u>Hadhi ya lugha</u>**.

*<u>Lugha rasmi.</u>*

Ni lugha inayopewa jukumu la kutumika kikazi mf katika

kuendeleza shughuli rasmi k.v elimu,

utawala n.k.

*Sifa za lugha rasmi*

· Hutumika katika mazingira au shughuli rasmi kv. Mkutano ya mawaziri,elimu, mikutano

ya machifu n.k

· Aghalabu huwa ni lugha inayosemwa nchini na pia nje ya nchi. Mf. Kiswahili.

· Inaweza kuwa lugha mojawapo ya wenyeji au lugha ya kigeni.

· Yaweza kutekeleza majukumu mengine k.v kuwa lugha ya Taifa.

· Huwa imesanifishwa na kusambazwa kupitia vyombo vya habari, vitabu na machapisho

mengine.

· Mara nyingi huwa ni lugha yenye historia ndefu.

· Iweze kutoa fursa ya kujiendeleza kimsamiati kutokana na kuibuka kwa maneno mapya.

· Huwa na msamiati mpana katika kila Nyanja za maisha. Isikosekane fasiri ya neno katika

lugha hiyo.

Majukumu.

· Kuendesha shughuli zote katika ofisi za serikali.

· Kufundisha shuleni(msingi hadi vyuoni).

*Lugha ya Taifa.*

Ni lugha iliyoteuliwa kama kitambulisho na ustaarabu wa taifa zima.

*Sifa za lugha ya taifa*

· Ina wazungumzaji wengi.

· Ina uwezo wa kutoa hisia za kikabila na kuwafunza watu kuhisi kuwa taifa moja.

· Huwapa watu utambulisho katika umoja wa mataifa.

· Huibua hisia za kizalendo miongoni mwa wananchi.

· Ni lugha ya mama/ kwanza ya kikundi cha watu katika taifa husika

o Ili wapokezane utamaduni, amali na historia.

o Ili wafunze wengine

· Iwe na muundo wa kiisimu unaofanana na ule wa baadhi ya lugha za watu katika taifa

husika hivyo kujifunza ni rahisi k.mKiswahili na lugha zingine za kibantu K.v kiluhya ,

Kikuyu n.k

· Iwe lugha mojawapo asilia, isiwe ya kigeni bali ya kienyeji; isilete chuki bali ieleze hisia

za uzalendo na utaifa.

*Majukumu.*

· Huunganisha watu wa taifa/huleta umoja.

· Huziba mipaka ya kikabila.

· Hukuza utamaduni wa kiafrika.

· Hukuza uzalendo wa watu wa taifa kwa kutumia lugha kama kifaa cha kuonyesha hisia

za kizalendo.

· Hutambulisha watu wa taifa fulani kwa mfano; wimbo wa taifa n.k.

· Huleta maendeleo ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kisayansi kutokana na umoja wa taifa

zima kilugha.

· Hufanikisha harakati za uongozi.

· Husawazisha watu kilugha kwa sababu hisia zitakuwa sawa.

*Lugha ya kimataifa.*

Ni lugha ambayo inaweza kutumika katika mawasiliano nje ya mipaka ya nchi husika kwa

masuala ya kisiasa, kidiplomasia, kibiashara na kitamaduni.

*Sifa za lugha ya kimataifa.*

· Ina uwezo wa kutimiza masuala ya kidiplomasia, kiuchumi, kisiasa, kielimu na hata sera

katika nchi mbalimbali.

· Ina uwezo wa kutumika katika vyombo vingi vya habari katika pembe nyingi duniani.

· Ina uwezo wa kutumika katika utafiti na uchunguzi kote duniani.

· Inasemwa katika pembe nyingin za dunia na watu wengi.

· Inatumika kuendesha mikutano na shughuli rasmi za kimataifa.

Majukumu ya lugha ya kimataifa.

· Hufundishwa katika vyuo vikuu vingi duniani- Amerika, Ujerumani, Uswidi, Uingereza,

Japani.

· Hutumika kutangazia na idhaa nyingi duniani kuanzia hapa Afrika ya mashariki,

Uingereza kuna BBC, voice of Amerika, Radio Urusi, Radio China kimataifa n.k.

· Kinasemwa katika kila pembe ya dunia mf. Afrika nzima, Amerika, China n.k

· Ni kati ya lugha mojawapo ya lugha zinazotumiwa kama lugha rasmi katika umaja wa

Afrika(AU).

· Hutumiwa katika kutolea magazeti mengi na majarida katika pembe tofauti za dunia.

Nchi kama vile Uchina, Ujerumani na Uajemi zina majarida yanayotolewa kwa lugha ya

Kiswahili.

*Viziada lugha.*

Ni matumizi ya ishara kv za mikono na uso mtu anapozungumza ili kusisitiza jambo Fulani.

*Sababu za kutumia viziada lugha.*

i. Haja ya msemaji kutilia mkazo analosema mfano kunao walio na tabia ya

kutupatupa mikono au kuwagusa wenzao wanapozungumza kwa nia ya kutilia

mkazo wanachokisema.

ii. Hali ya kihisia ya mzungumzaji - kwa mfano mtu akiwa na furaha au hasira

huathirika kupitia uso wake

iii. Haja ya kuwavutia au kuwanasa wasikizaji.

Aghalabu wazungumzaji bora huweza kunasa nadhari za wasikilizaji kwa kutumia

viziada lugha.

iv. Ukosefu wa muda wa kutosha

Huenda ikawa mzungumzaji ana muda mfupi sana wa kusema aliyonayo. Katika

hali hii mzungumzaji huona kuwa ni bora maneno yake yaandamane na ishara

v. Kudumisha siri

Ishara hutumika pale ambapo mzungumzaji anataka kusema jambo ambalo ni la siri

na hataki wengine wajue mf. Wanaovuta sigara hutumia ishara kuuliza kama

mwenzake ana sigara

vi. Ulemavu

Vigugumizi hulazimika kuambatanisha mazungumzo yao na viziada kwa sababu ya

kudodosa kwingi katika mazungumzo yao.

vii. Huwa ni jambo la kawaida kwa binadamu kuambatanisha mazungumzo na

matumizi ya viziada lugha.

*Dhana ya Lahaja*

- Ni vilugha katika lugha moja kuu( vijilugha vidogo vidigo vya lugha moja kuu)

- Ni tofauti za kimatamshi na maumbo pamoja na matumizi katika lugha ambayo

huhesabiwa kuwa lugha moja

- Lahaja huzungumzwa na kundi dogo ikilinganishwa na jumla ya watumizi wa lugha kuu

*Asili ya Lahaja (Sababu za kuzuka Kwa lahaja)*

(i) Kutawanyika kwa watu wanaotumia lugha moja ambao huenda kuishi maeneo

mbalimbali ambako mazingira ni tofauti

(ii) Kuingiliana na kuoana kwa watu na kwa hivyo kuathiri lugha kwa namna Fulani

(iii) Uhusiano baina ya watumiaji wa lugha kama vile wa biashara

(iv) Utawala na mfumo wa siasa tofauti ambao huweza kupendelea namna Fulani ya

lugha

(v) Dini kama vile Uislamu na ukristo, huweza kusababisha kuzuka kwa lahaja

(vi) Elimu husababisha kuzuka kwa lahaja ambapo aina Fulani ya lugha kama vile

Kiswahili sanifu ,hutumiwa katika mafunzo

(vii) Ujirani wa makabila. Makabila yanayopakana,lugha zao huweza kuathiriana kwa

kiwango cha kuzua lahaja mpya inayodhihirika kimatamshi

(viii) Mwachano wa kijiografia. Tofauti za kimasafa huweza kusababisha kuzuka kwa

lahaja.

(ix) Matabaka katika jamii. Tabaka la juu nhujizulia lahaja inayowatambulisha katika

matumizi ya misamiati na vilevile tabaka la chini

*Vipengele vinavotambulisha lahaja*

(i) Matamshi- maneno hutamkwa kwa namna tofauti katika lahaja tofauti

(ii) Msamiati

(iii) Sauti- sauti tofauti huweza kutumika katika lahaja tofautitofauti km, chiti na kiti,

moja/moya

(iv) Lafudhi tofautitofauti miongoni mwa lahaja

(v) Muundo wa maneno km. mtu/ mutu

(vi) Maana ya maneno- neon moja laweza kuwa na maana tofauti katika lahaja tofauti.

Km Lahaja 1: kufura-kushiba

Lahaja 2: kufura- kukasirika

*Umuhimu/matumizi ya lahaja*

(i) Hutumiwa katika kukuza lugha kwa kupanua msamiati wake kwa mfano, maneno

rununu, ngamizi na runinga ni za kilahaja

(ii) Hutumika katika kusanifisha lugha

(iii) Hudhihirisha utajiri wa lugha kupitia mitindo mbalimbali ya wazungumzaji

(iv) Hunogeza lugha kwa kutia kwa kutia ladha mazungumzo ya wasemaji mbalimbali

(v) Huwakilisha historia ya lugha

*Lahaja za Kiswahili.*

*Lahaja za kaskazini.*

(i) Kiamu – huzungumzwa Lamu

(ii) Kipate- huzungumzwa Pate kaskzini mwa Pwani ya Kenya.

(iii) Chimiini/chimbalazi- huzungumzwa Somalia katikati ya Mogadishu na kenya.

(iv) Kitukuu/kibajuni- huzungumzwa kaskazini mwa Pate na Lamu.

(v) Kisiu- huzungumzwa sehemu za Pate mjini Siyu.

*Lahaja za kati.*

(i) Kimvita- huzungumzwa Mombasa.

(ii) Kijomvu- huzungumzwa Jomvu.

(iii)Kingare- husemwa Mombasa(kilindini).

Lahaja za kusini.

(i) Kimtang'ata- Huzungumzwa Tanga, Pangani

(ii) Kipemba- Huzungumzwa Pemba.

(iii)Kimgao- huzungumzwa katika visiwa vya Kilwa.

(iv)Kingozi- Huzungumzwa Kismayu, Lamu kaskazini

(v) Kingazija- Huzungumzwa Ngazija (Comoro)

(vi)Chichifundi/chifundi- huzungumzwa shimoni.

(vii) Kiunguja- huzungumza Unhuja

(viii) Kimrima- huzungumzwa Tanga, Vanga, Pangani, Dar-es-Salaam

(ix)Kivumba- huzungumzwa Vanga,Wasini, Kusini mwa pwani ya Kenya

**Makosa katika lugha.**

*Sababu za makosa katika lugha.*

i. Athari ya lugha ya kwanza-ulefu/urefu

ii. Hali ya kiakili ya msemaji-mgonjwa au mlevi hudondosha sauti

iii. Kuhamasisha mafunzo na lugha moja hadi nyingine-katoto/kitoto

iv. Kutodhibiti mfumo n a ngeli katika lugha-ng'ombe hii/ng'ombe huyu

v. Kujumuisha kanuni za lugha :mnyambuliko wa vitenzi

soma-somesha

penda-pendesha(kosa)

vi. Kasi ya uzungumzaji huathiri usanifu wa lugha

vii. Kosa la kimakusudi-dhamira/lengo lakuwashawishi au kuburudisha

viii. Kosa la kutoelewa maana ya neno kimatumizi au umilisi wa maneno.Kudhani neno

‘tetesi’ linalo tokana na neno ‘teta’ ilhali maana yake ni uvumi.

***Sababu zinazochangia kufa kwa Kiswahili.***

i. Kiuchumi – maendeleo na ubunifu wa viwanda yanafanya watu kuhamia mijini. Watu

wanapohamia mijini wanaacha kuzungumza lugha moja na kuanza kuzungumza

nyingine kwa ajili ya mawasiliano

ii. Uchache wa wazungumzaji – idadi ya watu wanaozungumza lugha fulani inapopungua

lugha hiyo hufifia.

iii. Kutoungwa mkono na taasisi mbalimbali k.v elimu dini na vyombo vya habari

hukabiliwa na tisho la kufa

iv. Hadhi – lugha ambazo hazina hadhi kuishia kufa

v. Ndoa za mseto – watu wanapo changanyikana kupita ndoa za mseto husababisha lugha

zingine kudidima

vi. Kuhama kwa watu – kuhama kutoka sehemu moja hadi nyingine luga zao huathiriwa

vii. Hakuna sera maalumkutoka kwa serikali kuhusu matumizi ya Kiswahili.

viii. Kuna uhaba Mwingi/mkubwa wa waandishi

ix. Kuzuka kwa lugha ya sheng’ ambayo ni maarufu miongoni mwa vijana

x. Imani potovu kuwa lugha ya Kiswahili ni duni

xi. Kuzuka kwa lugha zingine k.v Kifaransa, Kiingereza

xii.Watumizi wa Kiswahili hawajali jinsi ya kutumia lugha

xiii. Ukosefu wa fedha za kufanya utafiti wa kina wa somo la Kiswahili

xiv. Kuwepo kwa sheria katika shule kuwa Kiswahili kizungumzwe siku moja kwa juma.

***Juhudi za serikali katika kuimarisha lugha ya Kiswahili.***

i. Kiswahili kufanywa lugha ya Taifa / rasmi

ii. Katiba ilipitisha Kiswahili kiwe lugha rasmi nchini

iii. Kiswahili kufanywa somo la lazima shule za upili / msingi

iv. Hutumika katika matangazo na taarifa za habari kupitia runinga

v. Viongozi wa dini wanahubiri wakitumia lugha ya Kiswahii

vi. Kenya na Tanzania zimeunda mabaraza ya vyama mbalimbali vya kushughulikia

maenezi k.v CHAKITA na BAKITA

vii. Lugha hii imetumiwa na wanabiashara.

viii. Lugha hii hufunzwa katika vyuo vikuu.

***Mkakati inayoweza kuchapuza kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya.***

i. Sera madhubuti - hii itaelekeza hatua za kupanga na kuendeleza lugha. Pia itabainisha

nyanja na maeneo ya matumizi ya Kiswahili.

ii. Kuamrisha Kiswahili - kitumiwe kama lugha ya kufundisha baadhi ya masomo, somo la

lazima n.k

iii. Ufadhili wa miradi ya utafiti.

iv. Maandalizi mema ya walimu na wataalamu wa Kiswahili.

v. Kubuni vyombo vya kukuza Kiswahili.

vi. Kusisitiza matumizi ya lugha sanifu.

vii. Serikali kufadhili uandishi na uchapishaji wa vitabu vya sarufi.

viii. Kuingiza Kiswahili kwenye kompyuta.

ix. Kuunda jopo la kitaifa la wataalamu - lengo lao ni kutoa mwongozo kuhusu Kiswahili.

x. Shughuli za sanaa, maonyesho na muziki

xi. Vitabu vingi kuchapishwa kwa lugha ya Kiswahili

xii. Shughuli za lazima bunge kuendelezwa kwa lugha ya kiswahili

xiii. Vyombo vya mawasiliao kutumia lugha ya Kiswahili

xiv. Kuunda jopo la kitaifa la wataalamu - lengo lao ni kutoa mwongozo kuhusu Kiswahili.

xv. Kuamrisha Kiswahili kitumiwe kama lugha ya kufundisha baadhi ya masomo, somo

lazima.

***Shughuli zilizochangia kuenea kwa Kiswahili kabla ya ukoloni.***

i. Biashara - Kiswahili kilifanywa lugha ya biashara kati ya pwani na bara.

ii. Sera ya lugha- Kiswahili kilifanywa lugha ya taifa nchini Kenya na Tanzania.

iii. Dini - Kiswahili kilitumika kusambaza dini za Uisilamu na Ukristo.

iv. Elimu - Wamishenari walitumia Kiswahili kufundisha, kuandika, kusoma, kuhesabu

na kazi mbalimbali za ufundi.

v. Utawala wa kikoloni- Sera ya lugha ya wajeremani nchini Tanganyika ilisisitiza

matumizi ya Kiswahili.

vi. Vyombo vya habari- magazeti mengi ya Kiswahili yalizuka nyakati za ukoloni.

vii. Siasa- Wahusika wengi katika vita vya ukombozi nchini Kenya na Tanzania

walitumia Kiswahili kama lugha ya mawasiliano.

viii. Hisia za utaifa miongoni mwa viongozi na wananchi zilichangia sana katika maenezi

maana watu waliwasiliana kutumia kiswahili.

ix. Utafiti - kina Steere na Kraph walifanya utafiti wa kina kuhusu Kiswahili na hata

kuandika vitabu.

x. Tamasha mbalimbali za muziki, drama na mashairi

xi. Uchapishaji wa vitabu, magazeti na majarida ya Kiswahili mfano kamusi

iliyochapishwa.

**Eleza jinsi vyombo vifuatavyo vimechangia katika kuenea kwa Kiswahili.**

*(a) Vyombo vya habari.*

i. Hutumia Kiswahili katika matangazo.

ii. Vipindi vya mashindano ambayo hutangazwa na vyombo.

iii. Huwasilisha makala mbalimbali wakitumia lugha ya Kiswahili.

iv. Huandaa makongamano ya waalimu wa Kiswahili.

v. Hukuza misamiati mipya ya lugha ya Kiswahili

*(b) Uchapishaji.*

i. Vitabu vipya ambavyo hukuza lugha ya Kiswahili vya kiada na ziada.

ii. Uchapishaji wa majarida na magazeti kuimarisha taaluma ya Kiswahili

*(c) Elimu*

i. Somo la lazima katika shule za msingi na sekondari.

ii. Hufunzwa hadi vyuo vikuu.

iii. Silabasi mpya ya Kiswahili ambayo inazumgumzia masuala ibuka kama teknolojia, jinsia

n.k

iv. Kuongezeka kwa waatalamna waalimu waKiswahili

*(d) Kuteuliwa kuwa lugha rasmi.*

i. Kutumika katika mikutano rasmi.

ii. Kutumika katika kuchapisha sera za serikali.

iii. Kutumika katika miktadha rasmi.

iv. kuendesha shughuli rasmi - mahakamani.

v. sKutumika katika makongamano ya kitaifa.

*Maenezi ya Kiswahili Afrika Mashariki punde baada ya uhuru yalikuwa na changamoto*

*tele. Fafanua zozote tano.*

i. Uhaba mkubwa wa wataalamu wa Kiswahili

ii. Athari kutoka kwa lugha ya kwanza.

iii. Watu kuchangamka lugha nyinginezo kama vile kiingereza, kijerumani.

iv. Imani potovu – lugha ya Kiswahili ni duni

v. Uhaba wa walimu wa Kiswahili.

vi. Uhaba wa vitabu vya Kiswahili.

vii. Kutokuwepo kwa sera ya lugha kutoka kwa baadhi ya serikali za mataifa ya Afrika

mashariki.

viii. Uhaba wa pesa za kutafiti.

ix. Nchi za Afrika za kukuza na kuendeleza Kiswahili.

**<u>Hali ya lugha ya Kiswahili nchini Kenya baada ya uhuru</u>**

i. Kiswahili kinafundishwa shuleni; kinatahiniwa kama somo la lazima katika shule za

msingi na sekiondari. Pia kinafundishwa katika vyuo vikuu

ii. Kinatumika katika utangazaji katika vituo vya utangazaji

iii. Ni lugha rasmi

iv. Serikali inatumia sambamba na Kiingereza katika kusambazia hati za serikali

v. Kinatumika kuendesha shughuli za kiutawala katika vituo vya

polisi, mahakamani n.k

vi. Kinatumika katika shughuli za kidini

vii. Kinatumika katika shughuli za sanaa, maonyesho na muziki.

viii. Wanasiasa wanakiona afadhali katika mikutano ya hadhara.

<u>**Chimbuko la Kiswahili**</u>.

Ni kufafanua namna Kiswahili kilivyoanza. Asili ya Kiswahili.

Taja nadharia tatu zinazoeleza chimbuko la kiswahili.

i. Kuwa Kiswahili ni lugha ya mseto.

Kiswahili ni tukio la maingiliano ya kibiashara, kijamii na hata kindoa baina ya wenyeji wa

Pwani na Waarabu.

Ø Haja ya Waarabu kuwasiliana na watumwa wao wa Kibantu ilisababisha kuchanganya

kwa maneno ya lugha za Kibantu na yale ya Kiarabu ili waweze kuelewana na hivyo

lugha lugha iliyochipuka ikawa ya Kiswahili(mchanganyiko wa Kibantu na Kiarabu.

Ø Shughuli za kibiashara-Waarabu walipofika kwa shughuli hizi hawakufika na wake zao

hivyo kulikuwa na uhaba wa wanawake wa Kiarabu hivyo wakaanza kufunga ndoa na

wanawake Waafrika na kupata watoto waliojifunza Kiarabu na Kibantu na lugha

iliyozungumzwa ikawa Kiswahili(lugha chotara-mchanganyiko wa Kiswahili na

Kibantu).

ii. Kuwa Kiswahili ni lahaja ya Kiarabu.

Ø Kuna idadi kubwa ya msamiati wa kiarabu katika kiswahili.

§ Ghadhabu – hasira.

§ Nadra -chache.

§ Tisa - kenda.

§ daima – milele.

Ø Lugha ya kiswahili imefungama sana na mafunzo ya dini ya Kislamu (ambayo ililetwa na

Waarabu toka Uarabuni). Vile vile miongoni mwa wale wanaojiita Waswahili ni wafuasi

wa dini ya Kislamu. Wao hutumia majina ya Kislamu kama vile Mohammed, Rehema,

Ramadhan n.k.

Ø Nyimbo za taarab hapo awali zilikuwa zikiimbwa kwa mashairi ya kiarabu na baadaye

zikaanza kuimbwa kwa mashairi ya Kiswahili.

iii. Kuwa Kiswahili ni lugha ya Kiafrika yenye asili ya kibantu.

Mtazamo hushikiliwa na wengi. Unashikilia kwamba Kiswahili ni Kibantukama vile

Kikamba, Kizulu, Kiganda n,k.

Tetea kauli kwamba Kiswahili ni kibantu.

Ø Maumbo ya maneno kwa Kiswahili na lugha za kibantu yana viambishi.

k.m mu-ndu.

m-tu

Ø Kuna mfanano wa kimsamiati katika lugha ya Kiswahili na lugha za Kibantu.

k.m kuhoa, korora, kooa.

Ulimi.lulimi

Ø Lugha ya Kiswahili mara nyingi huwa na muundo wa silabi wazi/huru. Mfumo huu vile

vile hudhihirika katika lugha nyingi za Kibantu.

Kikombe/shikombe.

Kitabu/shitapu.

Ø Nomino hupangwa katika ngeli kama tu ilivyo katika lugha nyingine za Kibantu.

A/WA Mtu anaenda.

Watu wanaenda.

M/A Mundu athi

Andu mathi.

Ø Upatanisho wa kisarufi ni sawa k.m Baba analima/Baba arima.

Ø Katika lugha za Kibantu kuna uwezekano wa kuunda maneno kutokana na aina nyingine

ya maneno. Mfano kuunda nomino kutokana na vitenzi.

Ø Mpangilio wa maneno katika tungo ni sawa.

Mtu anakuja leo/Mundu anecha juno

Ø Kuna mnyambuliko wa vitenzi katika lugha ya kiswahili jinsi tu ilivyo katika lugha

nyingine za Kibantu.

Lia – lilia/Rira – ririra.

Piga – pigwa/khupa- khupwa.

**Usanifishaji.**

Ni uamuzi wa kuchagua lugha moja au mojawapo wa lahaja za lugha na kuifanyia marekebisho

ya kimatamshi, kisarufi, kimaana, kimaandishi ili iweze kutumika katika shughuli rasmi.

Kusanifisha ni utaratibu wa kuondoa tofauti zote za lugha ambazo hutokana na kimaeneo na

tabaka.

***Sababu za kusanifisha Kiswahili*.**

*Kuwepo kwa lahaja nyingi za Kiswahili.*

Wingi huu wa lahaja ulitatiza sana mawasiliano katika shughuli za kibiashara, kielimu, n.k.

ambazo zilihitaji kuelewa kwa lahaja moja ili kueleweka na watu wote.

*Kulikuwa na hati tofauti zilizotumiwa kuandika Kiswahili.*

Mwanzoni kulikuwa na lahaja ya Kiarabu na baadaye Kirumi. Ni kutokana na hili ndipo

kulikuwa na tofauti katika kuendeleza maneno na kukawa na haja ya kutafuta namna moja ya

kuendeleza.

*Shughuli za kidini.*

Madhehebu mbalimbali yalijishughulisha katika shughuli za kidini na wote walijitahidi kutafsiri

biblia na nyimbo. Wamishenari hawa walitumia lahaja za maneno waliojikuta. Mfano CMC

walitafsiri wakitumia kimvita na University Mssion of Central Africa wakatafsiri wakitumia

kiunguja. Hii ilileta tofauti na ili kuondoa tofauti hii kukawa na haja ya usanifishaji.

*Haja ya kusawazisha maandishi ya kitaalamu.*

Wataalamu wa lugha walikuwa wameandika vitabu tofauti mfano kraph aliandika kitabu cha

Swahili Grammar(1850) katika lahaja ya Kimvita vilevile Steere akaandika kwa Kiunguja.

***Tofauti zilizotokea kwa maendelezo ya maneno na msamiati zilizua ugomvi kwa pande zote***

***mbili hivyo haja ya usanifishaji.***

*Haja ya kuwa na lugha moja ya mawasiliano na elimu.*

Hili lilifanyika baada ya kuteuliwa kwa Kiswahili kama lugha ya kufundishia, hata hivyo

kulikuwa na tofauti za matamshi na maendelezo hivyo haja ya kusanifishwa ili tuwe na lugha

moja.

*Uteuzi wa lahaja ya kusanifishwa.*

Kabla ya kuchagua na kusanifisha lahaja Fulani kulikuwa na mjadala mkali ulioibuka katika

mkutano kule Mombasa.

Lahaja ya kiunguja na kimvita ndizo zilikuwa na uzito mwingi hasa wa maandishi kuliko lahaja

zile zingine.

*Nguvu za Kiunguja*.

i. Ndiyo lahaja iliyokuwa imeenezwa sana na wafanyabiashara wa Unguja sehemu kubwa

ya bara ya Tanzania, Kenya na Uganda.

ii. Kiunguja kilitumika na watu wengi.

iii. Kiunguja kilikuwa kimefanyiwa uchunguzi na wataalamu.

iv. Kiunguja kilitumiwa sana katika masuala ya elimu na kidini.

v. Wepesi wake wa kutumika na lugha nyingine za kibantu.

*Nguvu za Kimvita*.

i. Kilikuwa na ukwasi wa msamiati na uwezo wa kuazima maneno kwa upesi.

ii. Kilikuwa na miswada mingi ya kifasihi, ushairi na dini.

iii. Kilikuwa bora katika maandishi ya nathari na usanifishaji.

iv. Kimvita kilikuwa cha kiwango cha juu zaidi kuliko Kiunguja.

*Udhaifu wa Kiunguja.*

i. Ilikuwa lugha ya biashara.

ii. Ilikuwa ya kiwango cha chini.

*Udhaifu wa Kimvita.*

i. Kilitumiwa zaidi sehemu za pwani na za Mombasa.

ii. Kilihusishwa na wakereketwa.

*Uteuzi wa Kiunguja.*

Waliounga mkono Kiunguja walikuwa na wakashinda baada ya kura kupigwa. Kiunguja

kiliteuliwa kuwa msingi wa kusanifisha Kiswahili kote katika Afrika Mashariki.

Ingawa Kimvita kilikuwa na utajiri, lahaja hii haikuwa imeenea.

**Kamati ya lugha na shughuli zake.**

Katika juhudi za kufanikisha upatikanaji wa maandishi kwa Kiswahili sanifu, nchi za Afrika

Mashariki ziliunda kamati ya lugha iliyojulikana kama Inter-Territorial Language Committee

mwaka wa 1930.

*Malengo ya kamati.*

i. Kusanifisha maandishi na kuhakikisha mtindo mmoja unazingatiwa.

ii. Kuchapisha vitabu.

iii. Kuwahimiza na kuwasaidia waandishi wa Kiswahili.

iv. Kuidhinisha vitabu vya kianda na vya ziada vinavyohitajika kufundisha shuleni.

v. Kuwapasha waandishi, habari zozote zile kuhusu njia tofauti au mitindo ya kusomeshea

katika kila nchi.

*Mafanakio ya kamati.*

i. Vitabu vingi vya sarufi, kilimo na hadithi vilichapishwa kwa mfano: Modern

Kiswahili Grammar.

ii. Tafsiri ilifanywa na vitabu kuchapishwa kwa Kiswahili kwa mfano: Kisima

chenye Hazina.

iii. Kamusi mbili zilichapishwa: Kiswahili - Kiswahili,Kiswahili - Kiingereza h.k

iv. Vitabu vingi vya kufundishia Kiswahili viliidhinishwa.

*Hatua za usanifishaji.*

i. Kuchagua lugha au lahaja moja ya usanifishaji miongoni mwa lugha au lahaja nyingi.

ii. Kuiweka hiyo lugha au lahaja katika maandishi ambako utaratibu wa kuendeleza

maneno huamuliwa na herufi zitakazotumiwa huchaguliwa.

iii. Kuipanua lahaja hiyo/lugha kimatumizi ambapo uamuzi hutolewa kuhusu mahali

lugha hiyo itakapotumiwa k.m redioni, magazetini, vitabuni na hata bungeni.

iv. Kuindeleza au kuikuza hiyo lugha kwa kutumia vyombo vya habari k.v redio,

runinga, magazeti n.k vile vile ikuzwe katika taasisi za elimu kwa kuiandikia vitabu

kuu mf. Kamusi.

**Sababu za ujenzi na upanuzi wa msamiati**

- Kukidhi mahitaji ya mawasiliano. Mazingira yanapobadilika, huhitaji msamiati mpya ili

kufanikisha mawasiliano

- Kupanua matumizi ya lugha katika Nyanja mbalimbali

- Kukuza msamiati wa lugha

- Kuendeleza lugha/ kikidhi hadhi ya lugha

- Kuzitafutia dhana mpya maneno.

- Kufidia msamiati unaopotea na kusahaulika.

**Njia za ujenzi na upanuzi wa msamiati**

(i) Kuunganisha maneno ili yaunde neon moja k.m nguvukazi, jopokazi nk

(ii) Kotohoa maneno kutoka lugha za kigeni k.m charger-chaja

(iii) Kuchukua maneno kutoka kwa lahaja za Kiswahili.

(iv) Kuchukua maneno kutoka lugha nyingine za kibantu

(v) Kuchukua maneno kutoka kwa lugha nyingine za kiafrika

(vi) Kuunganisha vipashiokwa mfano, Ukimwi- upungufu wa kinga mwilini

(vii) Kwa unyambulishaji

(viii) Upanuzi wa maana za maneno

(ix) Kutumia tafsiri sisi kwa mfano simu ya mkono- mobile handset, mama sukari- sugar

mummy

(x) Kuunda maneno kwa kutumia mbinu za kiisimu

**Mbinu za kuunda maneno**

- Kutohoa
- Tafsiri sisisi
- Kuunganisha maneno
- Uhamishaji wa maneno kutoka lugha mf. Ugali.
- Kukopa
- Tanakali za sauti
- Kuongeza viambishi / mnyambuliko.
- Ufupishaji / akronimu.

MAY YOUR HARD WORK BE A BLESSING TO YOU

EMAIL : PHELIXATAMBA@GMAIL.COM

CONTACT : 0742853219